Kwako bibi

Chagua kati ya chakula na kitenge cha siku kuu !

Nafasi tunakoishi o kutembelea, waonekana mambo nayotushangaza na utuvunja moyo. ati ya mambo hayo waweza kutaja huba anayo akina dada a mama kwa kuvaa itenge vipya akati wa karamu ma siku kuu. asaka, Noeli ao waka mpya vinapoka-ibia, baba wengi aanza tetemeka na upiga yohe wakiji-liza watafanya nini usudi wapate ununulia wake wao itenge vya siku uu. Si vibaya kuvaa vizuri wakati wa karamu lakini kinachotushangaza ni ile huba isiyo na mipaka. Watia pia mbali pato la mabwana wao wakisa-hau kuwa "kuku yakula kadiri ya midomo yake".

Mavazi wanayohitaji sana ni ile inayote-ngenezwa Uholanzi na ambayo wazoea kuita "Hollandais". Walalamika nafasi zote wakisema eti raha ya kuolewa ni kula na kuvaa vizuri. Ndipo pale wawatia mabwana zao lisani pembeni wakisema eti wao hawana saa za kuvaa nguo ambayo imekwi-sha kuonana na samaki zote za ziwa Kivu na kugeuka sawa vile kaungiyo. Niya yao ni kugeuka wa "mama kilo".

Wanapolazimisha wanunuliwa viatu na nguo za bei ghali wasahau kabisa kama chakula kina mafaa makubwa kwa kula na kujenga mwili. Wakubali kukosa chakula ingawa nyumbani kwao watoto wateswa na njaa ?

Ni wao pia msinji wa kubadilisha programa ya kuimari-sha maisha nyumbani.

Tamaa hiyo isyokuwa na mipaka yaleta mara kwa mara fujo nyumbani na kufikia hata kuwaangamiza watoto kwa kuwaletea magonjwa ya njaa kama vile bwaki kwani hawale namna inayotakika.

Wabwana wanaowaoa wabibi wa namna hiyo, wapata magumu kazini wakati wanapopokonya feza za mashirika wana-yoitumikia kusudi ya kutafuta na... ya kuwabembel... vimada vyao. Mwi... wao , ni kutu... gerezani am... wabaki kisha kupo... za kazi na kukim... liwa na bibi.

Wamama na wanaosoma maand... yetu watuto... maoni yao juu jambo hilo waki... mashauri muh... (important) inay... lekea wale wanaop... delea kuvaa pan... pa kupata cha... cha kujenga mwil...

Alamsiki

Soudan

Nimeiry amepinduliwa

Habari zinazoaminika kutoka Karthoum, mji mkuu wa Jamhuri ya Soudan zaeleza kuwa, bwana Ghaffar El Nimeiry hayupo tena raïs wa nchi hiyo. Amepinduliwa na bwana Abdel Haman aliyekuwa hapo hawali waziri wake wa ukingo wa raia.

Bwana Nimeiry alipata habari ya kupinduliwa kwake wakati alipokuwa akijitayarisha kupanda katika ndege kutoka Karo hadi nchini kwake. Wasaidizi wake wote walekwisha kunaswa. Wamoja wametupwa gerezani na wengine wasambishwa mbele ya waamzi kusudi ya kutoa nje harakati zao za kuangamiza raia wakipokonya feza bila woga wowote.

Punde kidogo tu kisha kujinyakulia madaraka huko Soudan, warugaruga wanaobaki kusini mwa nchi yake walianza kulalamika wakisema eti wamuomba awaachie raia (civil) madaraka. Na kama kukipita juma moja, wataanza fujo. Lakini kufuatana na masemi ya bwana Abdel Haman, ilionekana wazi kuwa hakuna fujo yoyote nchini humo na kuwa kwa sasa wakaaji wote wameanza kufanya kazi zao na kujitembeza kokote wapendako.

JUA

Gazeti la Kivu

Maniema

175.000 Z zimerudishwa katika sanduku la serikali

Kisha ziara ya siku tatu huko Kindu, mji mkuu wa wilaya ya Maniema, makamu wa liwali wa jimbo la Kivu, mwananchi Endjonga ambaye pia aongoza kamati ya uchunguzi wa malipo ya mishahara ya watumishi wa serikali amekwisha kurudi hapa mjini Bukavu. Kisa cha matembezi yake katika mawilaya ni kutaka kugundua wale walinda feza wanayo tabia mbaya ya kupokonya mishahara ya watumishi wa serikali. Mbele ya kujielekeza huko Kindu, aliwatia lisani pembeni walinda feza wa hapa Bukavu, Goma na Uvira.

Kisha uchunguzi mkali, mwananchi Endjonga na ujumbe wake waliweza kugundua kiasi cha zaïre 175.000 kwa mwezi tu wa tatu. Ni mwananchi Lubango Kumbele, pamoja na wasaidizi wake ndio waliokuwa na tabia hiyo ya kunyonya mishahara ya watumishi wa uwongo. Wengine walionaswa katika makosa hayo ni pamoja na wananchi Assani Kolokolo, Mushonio Banyimwire, Bibi Apendeki Mungomba, Amuri Mambo, Dunia Tchomba, Mwanapuungu Kitenop, Assani Lukeke, Yuma Songo, Mukaba Haridi, Tubassindji Baruani, Assani Selemani, Bushiri Kabbobo, Oluhun Engundu, Lukoja Kasala.

Jamaa hao walipelekwa mbele ya waamzi wa huko Kindu ili wapate kusamba makosa yao. Wale watakaoshindwa mbele ya waamzi ni lazima watupwe gerezani ambako watajuta makosa yao waki-kumbuka pombe ya "lumai mai" pamoja na samaki ya kambale.

Kwa ngambo yake, mwananchi Yambayamba, kiongozi wa chumba cha "fonction publique" pale Maniema aliachishwa kazi na kupelekwa mbele ya waamzi (juges).

Mwananchi Endjonga Bokwa Bomo'Wankoy, alifungua masikio ya wal... feza akiwaelezea ... bada ya siku si n... liwali wa jimbo la ... mwenyewe atatembele... niema kusudi ya k... ngua namna wanavyo... ka.

Kwa kumaliza aliw... waheshimu mambo Bab... taifa aliyonena k... hotuba yake ya t... 5 desemba 1984.

Tuzungumze

Adabu kwa kula chakula

Jirani yetu ni binadam, mtu yeyote ambaye anaishi mikoani ao vijijini, mtu haizuru nani bila ubaguzi wa rangi ama wa kabila. Kumbe tufanye vyote kusudi tuishi naye bila tatizo lolote. Hapa tunaendelea kuchapa maoni ya mwananchi Kimengele kuhusu jambo hilo.

Unapoitwa kwa jirani kwa kufurahi au kusikitika naye mara nyingi utaalikwa pia kula. Kwa ginsi yako ya kula au ya kunywa hutambua malezi ambayo ulipata nyumbani kwa wazazi, shuleni au katika maisha ya ujamii kwa jumla. Kumbe unapokuwa mikusanyoni au makundini mwa watu usiowafahamu bora unywe na ule kwa adabu. Usionyeshe kama unayo njaa ya mno na usijulishe kama chakula ulichoandaliwa kinakukuvuta kupita kiasi.

Usiwe na ubuge (pendo la kula kula) na usimeze kama mwenyi kukimbizwa. Unapojiandalia chakula usijaze sahani lako hata mipaka yake. Kwa mara ya kwanza twaa kidogo tu ili vyakula si vingi jirani naye apate kidogo. Wengine wote wakiisha kujiandalia unaweza kurudi tena.

Katika kula na kunywa utashi wetu wa kimtu hutambulikana ikiwa tunaonyesha kama hatupo watumwa wa chakula wala cha kunywa. Lakini tukijiachilia kuongozwa na misukumo ya kinyama mbele ya chakula au chakunywa mara hututia katika makundi ya watu bila utashi.

Chakula na kinywaji siyo ukomo. Ni misaada kwa kufika kwa ukomo. Tusivitumie kama vile Mungu wetu bali vitusaidie kupata ukomo wetu.

Siku tutakapofaulu kuongoza pupa ya kula au ya kunywa, ndio tutasema kama tumefanya ushindi mkubwa sana juu yetu sisi wenyewe binafsi. Pia mwenyi kujua kujikatalia katika kula na katika kunywa huyu anaweza kushinda pupa zingine na kukomesha vilema vyake vyote.

"Léopards" wangoja kusakanya "DIABLES ROUGE...

Wapendelevu wa mchezo wa kandanda kutoka Kinshasa na Brazzaville, watajielekeza kesho kunako uwanja wa tarehe ishirini mai (Stade du 20 mai) kwa kuhuzuria mchezo wa kanda kati ya majeshi ya Taifa ya Congo na Zaïre. Wananchi wanaobaki katika majimbo watafuata mchuano huo kwenyi televisheni na wengine kwa njia ya redio.

Tutakumbuka hapa kuwa katika mchezo wa kwanza, "Léopards" waliweza kusakanya "Diables Rouges" kwa kuichabanga mabao matano kwa mawili. Kufuatana na ushindi huo wa wanasoka wa nchi yetu mjini Brazzaville, wengi husema kuwa hakuna magumu ya kujipatia cheti cha kuendelea tena na michezo. Lakini kuna bado walakini !

Kwa kuwa michezo hiyo ni yenyi maana makubwa, viongozi wa shirika la mpira nchini mwetu na wale wa Jamhuri jirani ya Congo walibudi kuwa... waliokodishwa na ... ya huko Ulaya. K... kikundi cha Zaïre t... za kutaja kwa mfano ... ntubile Santos, Kab... Kiyika, Masengo, ... mbo. Wakongomani wa... ita pia wachezaji ... Martin, Ndomba Gé... na wengineo.

Kufuatana na ... tulizopokea, ina... kuwa wachezaji wetu ... tayari kufanya vyo... wezavyo kusudi ya k... tia ushindi hasa k... wa mchezo utaen... katika uwanja wetu ... fuatana na mchezo ... viongozi wa shiri... kandanda nchini ... waliamua kupeleka ... ndi chetu huko Lu... shi ambako lilipe... zoezi ya mwisho ... limu Makombo Ali ... ya kushtua Wakongo... Wakati tulipoku... mboni, wachezaji ... wamoja wa Zaïre ... wangali bado Ulaya ... ngoja ndege ya ... hadi Kinshasa. Tup... ka kuwa matokeo ... zo huo itakuwa ...